



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA



Kumb Na.MDC/

03.02.2022

YAH: TANGAZO LA KAZI YA KUJITOLEA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anapenda kuwatangazia nafasi ya kazi ya kujitolea kwa kazi ya wasaidizi wa watoto mahakamani kwa wakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Mbeya wa kata za Nsalala, Bonde la Songwe, Utengule Usongwe, Iwindi Inyala na Itewe, wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi za kujitolea za watoto mahakamani.

**WAS Aidizi wa Watoto Mahakamani
Sifa za Mwombaji**

1. Mwenye kuonesha upendo kwa watoto na anayezingatia haki na masilahi ya mtoto.
2. Mwenye uwezo mzuri wa kusikiliza, kuongea kwa kujenga na kupambanua hoja, awe na uwezo wa kusoma na kuandika vizuri,
3. Mwenye miaka 25 mpaka 59, wa kike au wakiume
4. Mwenye uwezo wa kufanya mahojiano na kuandika taarifa ya uchunguzi wakijamii na awe na uwezo wa kuwasilisha taarifa kwa maandishi na kwa mdomo
5. Awe raia mwema asiye na taarifa za makosa ya jinai.
6. Awe na uelewa wa mila, desturi na jiografia ya halmashauri ya Mbeya
7. Awe mkazi wa halmashauri na awe anapatikana angalau kwa muda mwingi ndani ya halmashauri ili kuwasaidia watoto pale mashauri ya watoto yaanapofika mahakamani au polisi
8. Mwenye kutunza siri, na awe tayari kuwasaidia watoto muda wote hata kutembelea familia za watoto.

Mwombaji anaweza kuwa mstaafu katika fani za ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, na walimu Wasaidizi wa msaada wa kisheria, waelimisha Rika, waliowahi kuwa wajumbe wa kamati za watoto wanaoishi mazingira hatari, wasaidizi wa mashauri ya watoto ngazi ya jamii (CCW), wasaidizi wa watoto polisi na raia mwema mwenye upendo na mapenzi mema katika kusimamia haki za watoto mahakamani.

KAZI ZA KUFANYA:

1. Kuwasaidia watoto kuweka shauri la mtoto kwenye taratibu za kimahakama pale mtoto anapokuwa ni shahidi dhidi ya mtoto mwenzake au dhidi ya mtu mzima.
2. kuhakikisha sauti ya mtoto inasikika vizuri mahakamani na kumhamasisha mtoto kushiriki kikamilifu katika shauri lake mahakamani.
3. kumsaidia mtoto aweze kujieleza juu ya mawazo na matamania yake kwa mahakama na kama mtoto hawezi kujieleza basi yeye aweze kueleza mahakama juu ya matamania ya mtoto.

Jengo la Ofisi ya Kata Inyala, S.L.P. 599 Mbeya, Simu : +255 734 189 769, Nukushi : +255 025-2500128,
Barua pepe: ded@mbeyadc.go.tz, Tovuti: www.mbeyadc.go.tz

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mkazi ya halmashauri ya wilaya ya Mbeya kutoka kata za Utengule Usongwe, Nsalala, Bonde la songwe, Iwindi, Mshewe, Inyala, Itewe, Tembela na Ijombe.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 25 mpaka 59 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote yaambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza *na ambatanisha barua ya utambulisho kutoka ofisi ya serikali ya kijiji/mtaa*
4. Maombi yote yaambatane na wasifu binafsi, vyeti vya mafunzo mbalimbali kama uliwahi kupata, kitambulisho cha Taifa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **28.02.2022** saa **9.30 Alasiri**. maombi yawasilishwe ofisi ya **Mkurugenzi Mtendaji Inyala**.
6. Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe awe na wadhamini wawili mwenye namba za simu na yaletwe masjala ya wazi ya **Mkurugenzi Mtendaji INYALA:**

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya,
S.L.P. 599,
Mbeya.**

Imetolewa na:



**Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya**

**K.m. Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya**